**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**MKOA WA SHINYANGA**

SHULE YA SEKONDARI MWELI
S.L.P 864,
USHETU –KAHAMA
**06.05.2026**

Simu namba:

**Mkuu wa Shule: 0754312379**

**Makamu Mkuu wa shule: 0765421483**

Unapojibu tafadhali taja: Kumb. Na: **UDC/MWL/01/2026**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………….………………

S. L. P. ………………………………………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MWELI, HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU MKOA WA SHINYANGA – 2026**

1. Ninafurahi kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya ……….**Shule ya Sekondari Mweli** ipo umbali wa Kilometa 70 kutoka mjini Kahama (nauli Tsh 8,000/=) Magari yanapatikana stand inayoitwa DODOMA-Kahama na kilometa 30 (nauli Tsh 5,000/=) kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Ushetu – **Nyamilangano**. Kituo cha kushuka ni shuleni Mweli Sekondari.

   Muhula wa masomo utaanza tarehe **…………..** Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kwa muda utakaopangwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

   **2.1 SARE ZA SHULE**

**Sare ya shule ni jukumu la Mzazi/Mlezi**

i. Sketi mbili kitambaa cha draft rangi ya bluu bahari ,dark blue na damu ya mzee **(Kitambaa namba 23**) mshono uwe wa linda boksi ndefu sentimita 30 kuanzia kwenye magoti kushuka chini. (**Mama Samia style**) wanafunzi waislamu wanaruhusiwa kuvaa ijabu,nusu kanzu ,na suruali kwa kuzingatia maadili ya dini ya kiislamu (zisiwe na Urembo wa aina yoyote ile wala kubana mwili)
ii. Rangi ya hijabu (Kijabu) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iii. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
iv. Sweta la rangi ya dark blue
v. Shamba dress (gauni refu) la rangi ya draft rangi nyeupe,dark blue na kahawia (**kitambaa namba 3)**.Mshono aina ya linda boksi.

**NB: SAMPULI YA KITAMBAA IMEAMBATISHWA**

vi. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu na viwe vya kufunga na gidamu (kamba).
vii . Soksi nyeupe ndefu za kutosha.
viii. Bukta moja na t-shirt moja nyeusi kwa ajili ya michezo (Samsung/Madrid/sports/adidas).
ix. Raba za michezo rangi nyeupe
x. Vitenge viwili vya kuogea (hairuhusiwi kuja na kanga)
xi. Nguo za ndani za kutosha
xii. Soksi ndefu za blue kwaajili ya michezo
xiii. Track suit ya dark bluu kwa ajili ya michezo (sumsung/adidas)
xiv. Shuka **mbili** rangi ya bluu na pinki (shuka za kimasai haziruhusiwi)
xv. Chandarua na blanketi moja (lisiwe na urembo)
xvi. Sweta rangi ya Kijivu kwaajili ya kusomea usiku.
xvii. Tai mbili za rangi ya kitambaa cha sketi.
xviii. T-shirt mbili za bluu bahari moja yenye shingo ya kola na moja isiyo na Kola

**NB: T-shirt pamoja na Tai zinapatikana Duka lililopo karibu na shule**

## KIELELEZO NA. 1: RANGI ZA SARE YA SHULE







## KIELELEZO NA. 2: SARE YA DARASANI JUMATATU-JUMATANO







## KIELELEZO NA. 3: SARE YA DARASANI SIKU YA ALHAMISI





**KIELELEZO NA. 4: SARE YA BWENINI (SHAMBA DRESS)**





**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo Mwanafunzi anapaswa kuja nayo Shuleni**

(i) Madaftari kumi (10) Counter Book 4 Quires, kalamu za kutosha na rula.

(ii) Ream mbili (A4) za karatasi kwa mwaka.

(iii) Box file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mitihani na spring file moja kwa ajili ya kumbukumbu binafsi ofisini.

(iv) **Non-Programmable Scientific Calculator (Kikokotoo)** kwa wanafunzi wanosoma masomo ya sayansi, jiografia na hisabati na **dissecting kit** kwa wanafunzi wanaosoma Biolojia.

Wanafunzi wanashauriwa kuwa na vitabu binafsi vinavyotumika kwenye tahasusi zao mfano Kamusi/Dictionary kwa masomo ya lugha pamoja na vitabu teule vya fasihi.

**VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU ANAVYOWEZA KUNUNUA NA KUJA NAVYO KULINGANA NA MASOMO NA CHEPUO WAKE;**

*1. Tanzania Institute of Education(2024). English for Advanced Secondary schools. Student's Book. Form Five*

*2. Tanzania Institute of Education(2024). Organic  Chemistry for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five and Six*

*3. Tanzania Institute of Education(2024). General and Inorganic Chemistry for Advanced secondary schools. Student's Book. Form Five and six*

*4. Tanzania Institute of Education(2024).  Practical geography for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five and six*

*5. Tanzania Institute of Education(2024). Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five*

*6. Taasisi ya Elimu Tanzania(2024). Kiswahili Shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha Tano*

*7. Tanzania Institute of Education(2024). Physics for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five*

*8. Tanzania Institute of Education(2024). Academic Communication for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Fivve*

*9. Tanzania Institute of Education(2024). Biology for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five*

*10. Tanzania Institute of Education(2024). Physical Chemistry for Advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Fivve*

*11. Taasisi ya Elimu Tanzania(2024). Fasihi ya Kiswahili kwa Shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha tano*

*12. Tanzania Institute of Education(2024). Business studies for Advanced Secondary Schools. Studen's Book. Form Five*

*13. Taasisi ya Elimu Tanzania(2024). Historia ya Tanzania na Maadili shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha Tano*

*14. Tanzania Institute of Education(2024). Literature in English for advanced Secondary Schools. Student's Book. Form Five*

*15. Tanzania Institute of Education(2024). Human Geography for Advanced secondary schools. Student's book. Form Five and Six*

*16. Tanzania Institute of Education(2024). Physical Geography for Advanced secondary schools. Student's book. Form Five and Six*

Kwa wanafunzi wa masomo ya lugha (kiswahili na English) vifuatavyo ni baadhi ya vitabu teule vya fasihi kwa masomo yote mawili kidato cha tano na sita;

**A. KISWAHILI**

**RIWAYA:**

1. Dunia Uwanja wa Fujo_ iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi;
2. Ua la Faraja_ iliyoandikwa na W. E. Mkufya;
3. Mirathi ya Hatari_ iliyoandikwa na C. G. Mung'ong'o; na
4. Wasifu wa Siti Binti Saad_ iliyoandikwa na Shaban Robert.

**TAMTHILIYA:**

1. Mukwawa wa Uhehe_ iliyoandikwa na M.M. Mulokozi;
2. Shujaa Mrambo_ iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo; na
3. Usaliti Mjini_ iliyoandikwa na Francis Imbuga.

**USHAIRI:**

1. _Fumbo Lililolala_ iliyoandikwa na Nyambari C. M. Nyangwine;
2. _Malenga wa Ziwa Kuu_ iliyoandikwa na Wallah Bin Wallah;
3. _Andamo, Msafiri Safarini_ iliyoandikwa na Mohammed Khelef Ghassani; n
4. _Wosia wa Baba_ iliyoandikwa na Ahmed Mohamed Amanzy.

**B. FASIHI YA KISWAHILI:**

**RIWAYA**

1. Vuta N'kuvute iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi;
2. Asali Chungu iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed;
3. Mwana wa Yungi Hulewa iliyoandikwa na Mohamed Said Abdulla; na
4. Vipuli vya Figo iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo.

**TAMTHILIYA:**

1. Kaptula la Marx_ iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi;
2. Nyerere na Safari ya Kanaani_ iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo; na
3. Morani_ iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo.

**USHAIRI:**

1. Dhifa iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi;
2. Utenzi Majumui wa Karne wa 21 ulioandikwa na Idd M. Mwimbe;
3. Malenga wa Bara iliyoandikwa n M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi; na
4. Fungate ya Uhuru iliyoandikwa na Mohamed Seif Khatib.

**C. ENGLISH LANGUAGE**

**C. ENGLISH LANGUAGE:**

**NOVELS:**
1. Animal Farm_ by George Orwell;
2. Chasing the Leopard Finding the Lion_ by Julie Wakeman-Linn.
3. The Opportunist Elite_ by Nyambari C. M Nyangwine; and
4. The Horizon Unveiled_ by Fellowes Mwaisela.

**PLAYS:**
1. The Government Inspector by Nikolai V. Gogol;
2. An Enemy of the People by Henrik Ibsen; and
3. A Taste of Heaven by Farouk Topan.

**POETRY**
1. Summons: Poems From Tanzania_ by Richard S. Mabala, et al, and
2. Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems_ by Jared Angira.

**D. LITERATURE IN ENGLISH**

**NOVELS:**
1. Arrow of God_ by Chinua Achebe;
2. A Man of the People_ by Chinua Achebe;
3. No Longer at Ease_ by Chinua Achebe;
4. Petals of Blood_ by Ngugi Wa Thiong'o;
5. A Grain of Wheat_ by Ngugi Wa Thiong'o;
6. Joy Comes in the Morning_ by Hopolang Phororo; and
7. The Lion of Yola_ by Severine Ndunguru.

**PLAYS:**
1. Betrayal in the City_ by Francis Imbuga;
2. I Will Marry When I Want_ by Ngugi Wa Thiong'o and Ngugi Wa Mirii;
3. Julius Caesar_ by William Shakespeare; and
4. Man of Kafira_ by Francis Imbuga.

**POETRY:**
1. Poets of Africa 7; Boundless Vouces Poem From Kenya by Arthur I. Luvai, and
2. The Bleeding Heart and Other Poems by Shilia Kaaya.

(v) Godoro dogo la "Sponge" lenye ukubwa wa **6' x 2½' x 4'**

(vi) foronya ya godoro moja (1) rangi ya Pink / bluu, na mto mmoja rangi ya Pink/bluu (kwa anayetumia mto).

(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

(vii) Ndoo 2 ndogo (lita kumi) zenye mifuniko.

(ix) Kwa Tahasusi za PCB na PCM waje na Jembe na mpini wake,fagio la ndani (soft broom),mopa(squeezer),brush ndogo ya choo (toilet brush) na ndoo moja ya lita 20.

Kwa Tahasusi za HKL, HGK na HGL waje na Jembe na mpini,fagio la nje ,mopa(squeezer) yenye raba siyo nyuzi pamoja na panga moja.

(x) Kanda mbili jozi moja kwa ajili ya kuogea.

(xi) Mswaki, dawa ya mswaki, sabuni za kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima, toilet paper tano (5).

(xii) Kabla ya kuingia shule hii utalazimika kupimwa na daktari aliyeajiriwa na Serikali. Fomu hiyo imeambatanishwa.Uje nayo shuleni ikiwa imekamilika.

(xiii) Uje na nakala ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (**results slip**).

(xiv) **URAIA**: Unatakiwa kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania au mkimbizi anayetambulika na Serikali ya Tanzania.Njoo na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya yako au **cheti chako cha kuzaliwa**.

(xv) **SHERIA ZA SHULE**: Sheria za shule zimeambatishwa na barua hii. Itabidi uzisome na kuzielewa ili uzifuate kikamilifu la sivyo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako. Kwa ujumla heshima (nidhamu), juhudi ya kazi na maarifa katika maisha ya shule ni msingi wa mafanikio. Moto wa shule – ***" EDUCATION IS THE KEY OF LIFE ".***

(xvii) **AFYA**. Mzazi unatakiwa kumkatia mwanao BIMA YA AFYA (bima kubwa ya NHIF) kwa ajili ya matibabu ya Tshs. 50,400 kwa mwaka.

(xviii) Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea Mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu aje nazo Mzazi/Mlezi anapomleta Mwanafunzi shuleni.

**2.3 Michango mbalimbali**

| **NA** | **Aina ya Michango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| **2.** | Tahadhari | 5,000/= |
| **3.** | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**Fedha zilipwe kwenye akaunti ya NMB namba 30601200164 MWELI SEKONDARI**

Na uje na **Bank pay- in-slip**.

Karibu sana Mweli Sekondari, shule yenye mazingira mazuri na tulivu ya kitaaluma

**DOROTEA CHRISTIAN NGONYANI**

**(Mkuu wa Shule)**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na**

**kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambayo ni Mwanafunzi ni Mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**

**Mkuu wa Shule: 0754312379**

**Makamu mkuu wa shule : 0765421483**

**Mwandamizi Taaluma: 0742502533**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayanzi

na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendashaji wa Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**.

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

(iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparations).

(iv)Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia Kikamilifu maelekekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mzingira ya shule

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(ix) Kutunza mali ya shule

(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari ; na

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**: Mwanafunzi hapaswi kuja na simu/wala kifaa chochote cha mawasiliano ya kielektroniki shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza kifaa/simu ya Mwanafunzi Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na Kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda

Kimoja kitatumika na Mwanafunzi mmoja tu; Mwanafunzi ataruhisiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba na Ugonjwa)

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na**:

(i) Wizi
**(ii)** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
**(iii)** Kugoma au kuhamasisha mgomo
**(iv)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
**(v)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
**(vi)** Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote na huruhusiwi kusuka nywele uwapo shuleni.
**(vii)** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
**(viii)** Uvutaji wa sigara.
**(ix)** Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
**(x)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria
**(xi)** Kubeba mimba au kutoa mimba
**(xii)** Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
**(xiii)** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
**(xiv)** Kudharau Bendera ya Taifa
**(xv)** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
**(xvi)** Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNLOJIA SHULE YA SEKONDARI MWELI FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE** (Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa Mkuu wa Shule)

Picha ya Mzazi/Mlezi

Picha ya Mwanafunzi

1. Jina kamili…………………………………………………………………
2. Tarehe ya Wilaya…………………………………………..
3.Utaifa………………………..………
4.Shule uliyohitimu kidato cha nne………………………………………………

**AHADI ZA MWANAFUNZI**

(a) Naahidi kutii na kuzifuata sheria zote za shule kama zilivyoambatanishwa.

(b) Naahidi kuwa sitathubutu kuanzisha wala kushiriki katika mgomo wa aina yoyote ile hapa shuleni.

(c) Naahidi kuwa nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa mbele ya uongozi wa shule endapo nitasikia tetesi au taarifa ya kuaminika juu ya jambo lolote linaloashiria kuleta vurugu au ukosefu wa amani shuleni. Pia nitafuata utaratibu wa kumaliza matatizo shuleni kwa kutumia vikao halali.

(d) Naahidi kutotoka nje ya eneo la shule kwa kipindi chote cha kuwepo kwangu hapa shuleni na kutokukaribisha mgeni yeyote kukaa ama kulala bwenini bila idhini ya uongozi wa shule.

(e) Naahidi kuwa sitavaa sketi na gauni fupi (Vimini), na nguo ambazo si sare ya shule (nguo za nyumbani) niwapo shuleni.

(f) Vile vile naahidi nitakula chakula kilichoandaliwa siku husika kutokana na utarabitu wa shule.

(g) Naahidi na kuamini kwamba dhumuni langu kuwa hapa shuleni ni kupata elimu na si vinginevyo.

(h) Naahidi nitafanya mazoezi yote, majaribio yote, mitihani yote ya nje na ndani (Mock and National Examination).

(i) Ninaahidi kuwa nitashiriki bila kukosa masomo ya usiku (Night Preparations) kufuatana na ratiba ya shule darasani kwangu.

Mimi……………………..………………………………………………………. Saini ………………………………..……Tarehe……………….…………

Baada ya kusoma kwa makini na kuelewa sheria za shule na ahadi za mwanafunzi zilizowekwa na Uongozi wa shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu pamoja na Mkuu wa Shule kuwa nitazitii; kuzingatia; kutekeleza na kufuata sheria zote za shule na kwamba nikizivunja sheria za shule nijihesabu nimejifuta shule mwenyewe.

Jina kamili ………………………………………..…………………..….

Saini ……………………………………….…… Tarehe …………………..……..

Jina kamili na sahihi ya Mzazi/mlezi wangu

……………………………………………………………….. saini………………………………

Tarehe ………………….

Namba ya simu ya mzazi/mlezi ……………………………………

Taja jina la mtu wa karibu ambaye shule inaweza kuwasiliana naye kwa jambo lolote iwapo mzazi/mlezi akikosekana;

Jina kamili………………………………………………………………………

Anwani…………………………………………….

Namba yake ya simu…………………..…………………

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**MWELI SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

To:

The Medical Officer

…………………………………………………..

…………………………………………………...

…………………………………………………..

Miss …………………………………………….…………………………………………

(Name in full)

Please examine the above named as to her physical and mental fitness for a full time training/studies.

The examination should include the following categories (i – ii) each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Primary/category iv will also render a girl candidate ineligible for the course:-

(i) (a) Eye-sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech

(e) Venereal disease (f) Leprosy (g) Epilepsy

(ii) Neuroses

(iii) Other serious diseases

(iv)Pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

(i)(a)Eye-sight.…………………………………………………………………………

(b)Hearing……………………………………………………………………..………(c)Limbs ……………………………………………………………………..…………

(d)Speech……………………………………………………………..……………….. (e) Venereal diseases………………………………………………………………

(f)Leprosy……………………………………………………….………………….. (g) Epilepsy………………………………………………………………………….

(ii)Neuroses ………………………..........................................................................

(iii)Serious diseases…………………………………………………………….

(iv)Pregnancy…………………………………………………………………………

Date…………………………………………. Signature ………………………………………

Station……………………………………… Designation ……………………………………

Official Stamp